SSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 45*** ***25th November, 2022***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette Of The United Republic Of Tanzania No 45 Vol.103 Dated 25th November, 2022*
Printed By The Government Printer, Dodoma By Order Of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 687 la tarehe 25112022

SHERIA YA TAASISI ZA KAZI,
(SURA YA 300)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 39(1))*

AMRI YA KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA YA MWAKA 2022

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kima cha Chini cha Mshahara ya Mwaka 2022 na itaanza kutumika tarehe 1 Januari, 2023.

Matumizi

2. Amri hii itatumika kwa wafanyakazi na waajiri wote katika sekta binafsi.

Tafsiri

3. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"kilimo" kitajumuisha uzalishaji wa mazao, shughuli za misitu, ufugaji na ufugaji wa wadudu, uchakataji wa awali wa mazao ya kilimo na wanyama unaofanywa na, au kwa niaba ya mwendeshaji wa shughuli hiyo pamoja na matumizi na ukarabati wa mashine, vifaa, zana na mitambo ya kilimo, ikijumuisha uchakataji, uhifadhi, uendeshaji au usafirishaji katika shughuli za kilimo ikihusisha Vyama vya Ushirika vinavyohusiana na uzalishaji wa kilimo;

"mikataba ya hali bora" maana yake ni makubaliano ya kimaandishi yaliyofikiwa na chama cha wafanyakazi kilichosajiliwa na mwajiri au chama cha waajiri kilichosajiliwa kuhusu suala lolote

la kazi;

"biashara na viwanda" inajumuisha ufanyaji wa biashara, utoaji wa huduma za kitaalam au shughuli zozote zinazofanana na hizo kwa lengo la kupata kipato, isipokuwa hazitajumuisha shughuli za uchimbaji madini na kilimo;

"wakandarasi" inajumuisha wahandisi wa ujenzi, majengo, mitambo, umeme na wakandarasi mahsusi;

"mfanyakazi wa kazi za ndani" maana yake ni mtu yeyote anayefanya kazi za ndani majumbani au katika kaya kwa malipo ya mshahara;

Sura ya 366

"mfanyakazi" ina maana iliyotafsiriwa katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini;

Sura ya 366

"mwajiri" ina maana iliyotafsiriwa katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini;

"nishati" inajumuisha michakato yote inayohusiana na uzalishaji au usambazaji wa nishati kutoka katika chanzo chochote;

"makampuni ya kimataifa" maana yake ni mashirika ya kimataifa au makampuni ya biashara ya kimataifa yanayojihusisha na biashara katika nchi mbalimbali;

Sura ya 123

"shughuli za uchimbaji" zitakuwa na maana kama zilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Madini, na hazitahusisha shughuli yoyote inayohusiana na uzalishaji wa chumvi au chokaa;

"mfanyabiashara mkubwa" maana yake ni mtu yeyote anayefanya shughuli za kiuchumi zenye uzalishaji mkubwa na faida kubwa;

"sekta binafsi" maana yake ni sekta yoyote isipokuwa sekta ya umma;

"kampuni ndogo" maana yake ni kampuni zote isipokuwa kampuni kubwa au za kimataifa;

"hoteli kubwa au za kitalii" maana yake ni hoteli zote zinazoendeshwa kwa kiwango cha juu na faida kubwa zikiwemo kambi zinazotoa malazi na huduma nyinginezo kwa watalii.

Sekta na maeneo

4.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Amri hii, sekta na maeneo ya kima cha chini cha mshahara yanaanzishwa kwa utaratibu uliowekwa katika Jedwali la Kwanza la Amri hii.

(2) Ukokotoaji wa viwango vya mshahara vinavyolinganishwa kwa kuzingatia saa, siku, wiki, wiki mbili au mwezi, utaamuliwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza lililotolewa chini ya kifungu cha

Sura ya 366

26(1) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini.

(3) Kiwango cha kima cha chini cha mshahara kilichoainishwa katika Jedwali la Pili kitachukuliwa kuwa kiwango cha chini kinacholipwa kwa mfanyakazi katika sekta au eneo husika, na mwajiri anaweza kumlipa mfanyakazi huyo zaidi ya kima cha chini isipokuwa hatamlipa mfanyakazi chini ya kiwango kilichowekwa katika sekta au eneo husika.

(4) Viwango vya kima cha chini cha mshahara vinaweza kuboreshwa kupitia mikataba ya hali bora au vinginevyo.

Viwango vya ajira

5.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Amri hii, viwango vya ajira vinavyotumika kwa wafanyakazi wote katika kila sekta au eneo lililoainishwa vitakuwa kama vilivyoainishwa chini ya Sehemu ya III ya

*Tangazo la Serikali Na. 687 (Linaendelea)*

Sura ya 366

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, au kama inavyotekelezwa katika mikataba ya ajira na mikataba ya hali bora.

(2) Pamoja na likizo ya mwaka yenye malipo, mfanyakazi atakuwa na haki ya posho ya likizo mara moja katika kila miaka miwili ya utumishi endelevu kwa mwajiri yuleyule.

(3) Mwajiriwa atastahili posho nyingine kama ilivyokubaliwa katika majadiliano kati ya mwajiri na mwajiriwa.

(4) Bila kujali ujumla wa aya hii, dereva wa lori atastahili posho kwa ajili ya umbali wa safari, kukaa zaidi nje ya kituo cha kazi, upakiaji na ushushaji wa mizigo kama ilivyokubaliwa katika majadiliano kati ya madereva na waajiri.

Wafanyakazi wanaopata maslahi bora

6. Endapo wakati wa kuanza kutumika kwa Amri hii, mfanyakazi yeyote anayepokea mshahara wa kiwango cha juu na masharti bora ya kazi kuliko yale yanayotolewa chini ya Amri hii, mfanyakazi huyo ataendelea kupokea mshahara wa kiwango cha juu na masharti bora ya kazi, ikiwa ameajiriwa na mwajiri huyo huyo.

Kufutwa TS. Na. 196 la 2013

7. Amri ya Kima cha Chini cha Mshahara ya Mwaka 2013 inafutwa.

---

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

SEKTA NA MAENEO YA KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA

(a) Sekta ya kilimo;

(b) Sekta ya afya;

(c) Sekta ya mawasiliano;

(d) Kazi za majumbani na hotelini;

(e) Huduma za ulinzi binafsi;

(f) Sekta ya nishati;

(g) Sekta ya usafirishaji;

(h) Sekta ya ujenzi;

(i) Sekta ya madini;

(j) Huduma za shule binafsi;

(k) Sekta ya biashara na viwanda;

(l) Sekta ya uvuvi na huduma za baharini;

*Tangazo la Serikali Na. 687 (Linaendelea)*

(m) Sekta nyingine

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(3))*

VIWANGO VYA CHINI VYA MSHAHARA

| | Sekta na Maeneo | Muda | Kiwango (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1. | Sekta ya kilimo | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 718<br>5,385<br>32,310<br>64,620<br>140,000 |
| 2. | Sekta ya afya | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,000<br>7,501<br>45,003<br>90,007<br>195,000 |
| 3. | Sekta ya mawasiliano | | |
| | (a) Huduma za mawasiliano | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 2,564<br>19,232<br>115,394<br>230,787<br>500,000 |
| | (b) Huduma za utangazaji na vyombo vya habari, posta na usafirishaji wa vifurushi | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,154<br>8,654<br>51,927<br>103,854<br>225,000 |
| 4. | Kazi za majumbani na hotelini | | |
| | (a) wafanyakazi wa kazi za ndani walioajiriwa na wanadiplomasia na wafanya biashara wakubwa | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,282<br>9,616<br>57,697<br>115,393<br>250,000 |
| | (b) wafanyakazi wa kazi za ndani walioajiriwa na maafisa wenye stahiki | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,026<br>7,693<br>46,157<br>92,315<br>200,000 |
| | (c) wafanyakazi wa kazi za ndani, isipokuwa wale walioajiriwa na wanadiplomasia, wafanyabiashara wakubwa na maafisa wenye stahiki wasioishi katika kaya ya mwajiri | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 615<br>4,616<br>27,694<br>55,389<br>120,000 |
| | (d) wafanyakazi wa kazi za ndani wengine wa nyumbani ambao hawajaainishwa katika aya (a), (b) na (c) hapo juu | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 308<br>2,308<br>13,847<br>27,694<br>60,000 |
| | | | |

*Tangazo la Serikali Na. 687 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (e) hoteli kubwa au za kitalii | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,539<br>11,539<br>69,236<br>138,472<br>300,000 |
| | (f) hoteli za kati | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 923<br>6,924<br>41,542<br>83,083<br>180,000 |
| | (g) migahawa, nyumba za kulala wageni na baa | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 769<br>5,770<br>34,618<br>69,236<br>150,000 |
| 5. | Huduma za ulinzi binafsi | | |
| | (a) makampuni makubwa na ya kimataifa | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,139<br>8,539<br>51,235<br>102,469<br>222,000 |
| | (b) makampuni madogo | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 759<br>5,693<br>34,156<br>68,313<br>148,000 |
| 6. | Sekta ya nishati | | |
| | (a) makampuni ya kimataifa | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 3,036<br>22,771<br>136,626<br>273,252<br>592,000 |
| | (b) makampuni madogo | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,154<br>8,654<br>51,927<br>103,854<br>225,000 |
| 7. | Sekta ya usafirishaji | | |
| | (a) huduma za usafiri wa anga | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 2,000<br>15,001<br>90,007<br>180,014<br>390,000 |
| | (b) huduma za utoaji mizigo na usambazaji | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,846<br>13,847<br>83,083<br>166,167<br>360,000 |
| | (c) huduma za usafiri nchi kavu | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,539<br>11,539<br>69,236<br>138,472<br>300,000 |
| 8. | Sekta ya ujenzi | | |
| | (a) Wakandarasi Daraja la I | Saa<br>Siku | 2,154<br>16,155 |

*Tangazo la Serikali Na. 687 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 96,931<br>193,861<br>420,000 |
| | (b) Wakandarasi Daraja la II - IV | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,846<br>13,847<br>83,083<br>166,167<br>360,000 |
| | (c) Wakandarasi Daraja la V-VII | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,641<br>12,309<br>73,852<br>147,704<br>320,000 |
| 9. | Sekta ya madini | | |
| | (a) wenye leseni za uchimbaji na utafutaji madini | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 2,564<br>19,232<br>115,394<br>230,787<br>500,000 |
| | (b) wenye leseni za wachimbaji wadogo | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,539<br>11,539<br>69,236<br>138,472<br>300,000 |
| | (c) wenye leseni za wafanyabiashara | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 2,308<br>17,309<br>103,854<br>207,708<br>450,000 |
| | (d) wenye leseni za madalali | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,282<br>9,616<br>57,697<br>115,393<br>250,000 |
| 10. | Huduma za shule binafsi (awali, msingi na sekondari) | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,062<br>7,962<br>47,773<br>95,546<br>207,000 |
| 11. | Sekta ya biashara na viwanda | | |
| | (a) biashara na viwanda | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 769<br>5,770<br>34,618<br>69,236<br>150,000 |
| | (b) taasisi za fedha | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 3,036<br>22,771<br>136,626<br>273,252<br>592,000 |
| 12. | Sekta ya uvuvi na huduma za baharini | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 1,221<br>9,155<br>54,927<br>109,855<br>238,000 |
| | | | |

*Tangazo la Serikali Na. 687 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. | Sekta nyingine ambazo hazijaainishwa katika Amri hii | Saa<br>Siku<br>Wiki<br>Wiki mbili<br>Mwezi | 769<br>5,770<br>34,618<br>69,236<br>150,000 |

Dodoma,
16 Novemba, 2022

JOYCE L. NDALICHAKO
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu*